*jiwe la kujengea la kiroho na 16*

**HIVI SASA TUNATAWALA PAMOJA NA KRISTO**

***Warumi 5:17 kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya Yule mmoja Zaidi sana wao wapokea wingi wa neema,na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa Yule mmoja Yesu Kristo.***

‘’Nakufanya kuwa ufalme na makuhani wa Mungu naye ni Baba yetu, utukufu na ukuu una yeye hata milele na milee Amina**.”[Ufunuo 1:6]** yeye ametufanya sisi ! oh kuna kweli nyingine inabidi tuzitilie mkazo.Na hii ni moja wapo. Yeye! Yeye anatufanya sisi! Wokovu ni utendaji wake . Wokovu ni wa Bwana. Wote ni neema. Ametukomboa sisi kwa kusudi. metununua sisi kwa kusudi sisi ni wafalme, wafalme wa kiroho ***(1Petro 2:9-10)*** oh, tutaenda kuwa wafalme hapa duniani pamoja naye atakapo keti katika kiti Chake (Ufunuo 3:21) lakini sasa hivi sisi ni wafalme wa kiroho na tunatawala juu ya ufalme wa kiroho. [1]

Ufalme wa Mungu siyo wa dunia hii,ufalme wa Mungu umo mioyoni mwetu.Yesu alisema ufalme wa Mungu unakuja,lakini sio posipo nguvu [matayo 16:16] Na ufalme wa Mungu uko kati yenu ***(Luka17:21).***Roho Mtakatifu,ufalme wa Mungu ukitanda ndani ya mtu na kuongoza na kumtawala yeye huo ni ufalme. [2]

Sasa Adamu alikosa kwa kusikiliza haja za mkewe, badala ya kusikiliza Neno la Mungu hicho ndicho kilicho mfanya Adamu atende dhambi. Mke alifanya mahojiano na shetani, na halafu akazalisha zao/tunda kwa Adamu. Adamu akaliacha Neno na kuliuza.Alipoteza urithi wake pia alipoteza ushirika wake na hali ya uzima.kumbuka “siku utakapokula hayo siku hiyo utakufa” ***(Mwanzo2:17).*** Na hapo alipopoteza uzima wake alipoteza na urithi wake katika maisha kwa sababu alikuwa na mamlaka kamilifu ya utawala wa dunia. Ali kuwa ni mungu wa dunia, Mungu ni Mungu wa ulimwengu wote kila mahali. Lakini mwanae alikuwa na hii dunia chini ya mamlaka yake mwenyewe. Angeweza kunena, angeweza kuvipa vitu vingine ,angeweza kusema; angeweza kusimamisha maumbile angeweza kufanya chochote alichotaka kufanya.Unaona? kalini alipofanya hivyo alipoteza urithi wake.[3]

Katika ***Wakoiosai 1:13”***Naye ametukomboa katika nguvu ya giza,alituhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake”.Sasa hivi tuna tawala pomoja na kristo,tukitawala na watawala juu ya dhambi,dunia,mwili na shetani. Kuzitangaza sifa zake utukufu; alijionyesha yeye mwenyewe kwa maana ni kristo ndani yete [***Wakolosai1:26_27***] Alipenda na kutenda sawa na mapenzi yake. Ndivyo hasa hata sasa tumeketi pamoja na kristo katika mazingira ya kimbinguni ndani ya kristo.

***(Ufunuo 2:6)*** “na kutufanya ukuhani”. Ndiyo, makuhani kwake yeye tukimtolea sifa za rohoni na za midomo iliyotakaswa. Tukitumia muda wetukama dhabihu safi ya kupendeza kwake. Tukimwabudu katika kweli na roho ***(Yohana 4:23-24).***

Tukifanya maombi na upatanisho ***(Rumi 8: 26-27)*** makuhani wafalme kwa Mungu wetu, sio ajabu dunia haipendezi kwetu, na sisi ni watu wasio wa kawaida walio na bidii katika kazi njema ***(Waebrania 10:23-24)*** tumeumbwa katika yeye tuwe wana kama vile baba yetu. [1]

Sasa kiti cha enzi cha kwanza kilikuwa mbinguni, kiti cha hukumu, kiti cha pili cha enzi ni kuwa ndani ya Kristo, kiti cha enzi cha tatu ni ndani ya mtu.

Ni wangapi wanajua hilo? Angalia Mungu anavyoliendea. Moyo wake ni nini? Unakumbuka ujumbe wangu. Mungu alichagua moyo wa mtu kuwa mahali pake pa kumuongoza! Shetani alichagua kichwa chake kuwa mahali pake pa kuongozea; unaona, unamfanya aone mambo, kupitia macho yake atazame, lakini Mungu katika moyo wake anamfanya mtu aamini mambo ambayo hayaoni. ***(Waebr 11:1,6)*** unaona, Mungu yuko katika moyo , katika moyo wa mtu, sehemu ya kwanza ya mtu ni mwili, sehemu inayofuata ni nafsi yake, ambayo ni asili ya Roho ambayo inamfanya vile alivyo.

Alipoendelea sasa, sehemu ya tatu ya mtu ni Roho yake iko katikati ya moyo wake, na ndani kule katikati ya moyo ndipo Mahali Mungu anapokuja kwa ajili ya kiti chake cha enzi [4]

Yeye ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu juu ya kiti cha enzi cha Mungu (Rumi 8:34) hicho siyo kiti chake cha enzi yeye anarudi kuja kutawala katika kiti chake cha enzi. Ni kile kiti cha enzi cha Daudi. Yeye atachukua kiti chake cha enzi. Yeye ameketi katika kiti cha enzi cha Mungu***.(Ufunuo 3:21)*** akisubiri mpaka adui wa mwisho atakapowekwa juu ya miguu yake.(wafilipi 2:3-11). Siku moja yeye atarudi akija pamoja na zile nafsi za thamani pamoja naye. Ili zichukue kutokuharibika au nhali ya kutokufa, kuishi katika mwili wa utukufu, kuishi wakati wa utawala wa miaka elfu, na baadae milele pamoja naye. [5]

Tazama Kristo ndani yako inamfanya yeye awe kiini cha maisha ya ufunuo. Unaona? Kristo ndani yako inamfanya yeye awe kiini cha ufunuo ***(Kolosai 1:26 – 28).*** Kristo katika Biblia iwe ufunuo mkamilifu wa Kristo. Kristo ndani yake inakufanya wewe uwe ufunuo mkamilifu wa kitu chote, unaona, kile Mungu anachojaribu kufanya.

Ni nini basi kule kuzaliwa mara ya pili? Unaweza kusema “Vema huku kuzaloiwa upya maana yake ni nini? Ni kule kufunuliwa kwa Yesu kristo kibinafsi kwako. Amina! Unaona? Siyo umejinga na kanisa, umepeana mikono, umefanya kitu Fulani tofauti, umesema.

Kanuni Fulani, umeahidi kuishi kwa taratibu Fulani za kisheria. Lakini Kristo, Biblia, Yeye ni lile neno lililofunuliwa kwako na haijalishi mtu yoyote atasema nini. Kile kinachoweza kutokea , Ni Kristo, mchungaji, kuhani, chochote kinaweza kuwa , ni kristo ndani yako, huo ndio ufunuo ambao kanisa hujengwa katika huo. ***(Mathayo 16:17-18)*** na neno linapofunuliwa linajieleza lenyewe.

Kule kuzaliwa upya ni Kristo, ni ule ufunuo. Mungu ameifunua ile siri kuu, na hiyo nikuzaliwa upya, sasa utaenda kufanya nini pale utakapoliweka lile kundi lote pamoja, ambapo ule ufunuo unakubaliana sawa kabisa, na Mungu alilieleza hilo kupitia neno lake kwa kulidhihirisha. Oh kama kanisa lingelijua tuu nafasi yake! Litajua, siku moja . Hapo sasa utatokea litakapotambua kile kilicho. [16]

Sisi sote tunaamini juu ya kuja kwa Bwana. Kwamba yeye atatokea, kwa kuona hilo, tunataka kuweka kila nguvu yetu tuliyo nayo jinsi ya kuendeleza ufalme na kumpatanyule mtu wa mwisho aweze kuokolewa awe ndani ya ule ufalme. ***(1Kor 12:13)*** na Yule wa mwisho atakapookolewa hatutakuwa na mwingine zaidi. Itakuwa tuu kiasi Fulani tuu. Na Yule wa mwisho natakapoingizwa ndani, mwili wa Yesu kristo utakuwa umekamilika, ule unyakuo utatokea, na kwa hiyo tunaitamani sana siku hiyo ili tuondolee hapa mahali ambapo tunaishi sasa. Kwa maana ni uhakika ninyumba ya wadudu, tunajua hilo, iliyojaa maumivu, magonjwa na mambo ya kuvunja moyo, na matatizo ***(Wafilipi 3:20:20-21)*** Na jamani nani atapenda kukaa hapa. Wakati kuna mahali pazuri pa kwenda kukaa? ***(Kor 5:1-8)***

Kwa hiyo tunajaribu kuifanya kila nafsi iokolewe, ili kwamba Yesu kristo aweze kuja . na hawezi kuja mpaka lile jina la mwisho lililoko kwenye kitabu cha uzima ambalo liliwekwa pale kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (ufunuo 13:8) Jina hili litakapoitwa hilo ndilo sasa la mwisho, amekuja kuokoa, "kukirudisha mahali pake pa kwanza" na atakapomleta ndani Yule mmoja ambaye ni wa mwisho… yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu leo akifanya kazi ya upatanisho ***(Waebr 4:14-16)*** Na ile nafsi ya mwisho itakapookolewa, ambayo ilikombolewa ambayo Mungu aliiona na kuifahamu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ile nafsi ya mwisho unapookolewa, ile inafunga kile kitabu. Hapo mwanakondoo anatoka na kuchukua kile kitabu katika mkono wa kuume way eye aliyeketi kwenye kiti cha enzi (ufunuo 5P:6-10) hapo sasa anakuja, anakuja duniani. [7]

Alikuwa analithibitisha hilo……. Alipasua mwili wa Yesu vipande, alichukua kwa roho. Akauinua mwili mpaka mkono wa kuume wa kiti cha enzi wa Mungu. Na akaituma huku chini ile sehemu nyingine, ile sehemu aliyoimega itoke, yulre Roho aliye juu yetu, ambayo inaitwa Roho mtakatifu, na uhai Yule hasa ambao ulikuwa ndani ya Kristo uko ndanni yako. Hiyo inaonyesha yeye ni mkombozi wako, yeye amekuasilisha wewe kuwa wa Mungu, na sasa sisi ni wana wa binti wa Mungu, tukiwa na Roho wa kristo. (rumi 8:15 – 16, Wagalatia 4: 1-7)Amina [8]

Kila kitu katika Biblia kipo katika utatu. Unajua hilo, nikasema "hata wewe uko katika utatu, nafsi, mwili, na Roho" Unaishi katika utatu. Jikoni, seebuleni, chumba cha kulala, unaweza ukawa navyumba nane au kumi tofauti. Lakini unaishi katika vyumba vitatu. Mungu baba, mwana na roho mtakatifu katika utatu. Na tutaona ya kuwa kule kuja kwa kristo kuko katika utatu. Alikuja kwanza kumuokoa Bibi arusi wake, anakuja tena kumchukua bibi arusi wake, halafu anarudi pamoja na bibi arusi wake. Kamamfalme na malkia. Kwa ajili ya kutawala katika utawala wa miaka elfu. (**Ufunuo 19:11-16)** unajua hilo kwamba kila kitu kipo katika utatu. Na sisi tuko katika utatu, yunayo miili inayokufa, tunayo miili ya kimalkia na kimbinguni nahalafu miili ya utukufu. Hatua tatu zinatuleta tena kwenye ukamilifu tena kama ilivyokuwa edeni. [9]

Anapokuja sasa, yeye ni kuhani, alipokuwa hapa duniani yeye alikuwa ni nabii, nabii wa Mungu sasa amechukua damu yake mwenyewe na akaenda kwa Baba ***(Waebr 9:11-14)*** ambalo linamfanya yeye kuwa kuhani. Atakaporudi tena atakuwaa mfalme. Nabii, kuhani na mfalme, alikuwa nabii wa Mungu, alikuwa Tai. Alikuwa kuhani wa Mungu alikuwa mwanakondoo, atakaporudi tena atakuwa Yle samba ***(Ufunuo 10:1-3) Yule*** mfalme (wa kabila la Yuda) ili kutawala [10]

Yuko wapi Yule atakayepanda mbegu kwa ajili ya kanisa lile la wakati wa mwisho. Iko wapi ile mbegu iliyoiva. Yule Eliya aliyeahidiwa? Ni mara tu baada ya siku zake ile dhiki kuu itaanza na kuichoma moto dunia.

Na baada ya kurudi kwa kanisa la bibi arusi na kristo watawakanyaga/ watatembea juu ya majivu yao katika utawala wa miaka elfu. ***(Malaki 4:1-3)*** waakati dunia itakapotakaswa kwa moto. Na hapo watatawala . na wapagani ambao walikuwa hawajasikia injili watafufuliwa katika wakati huo. Na wana wa Mungu watadhihirishwa. ***(Warumi 8:19-23)*** kama atatawala ni budi awe na watu ambao atawatawala, atakuwa na himaya, watatawala na kumiliki pamoja na kristo. ***(2Timotheo 2:11-13)*** na Kristo atatawala kwa fimbo ya chumayale mataifa. (ufunuo 2:26-28)halafu udhihirisho wa wana wa Mungu wakiwa na kama yale aliyokuwa nayo wakati alipokuwa hapa, hapo sasa utakuwepo utawala wa miaka elsu katika ule utawala.
(***Isaya 65:17-25, Rumi 8:18-24, Ufunuo 20:4-6)*** [11]
Sababu iko katika warumi 8:17-18 "na kama tu watoto basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithi pamoja na kristo, naam tukiteswa pamoja naye ili tupate kutukuzwa pamoja naye, kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuw si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu"

Inapasa tuteseke pamoja naye vinginevyo hatuwezi kutawala pamoja naye. Unapaswa uteseke ili uweze katawala. Sababu ya hili ni kuwa, tabia haiwezi kujengwa bila ya mateso. Tabia ni ushindi, siyo karama/ kipawa. Mtu asiye na tabia hawezi kutawala kw asababu nguvu bila tabia ni ushetani, lakini nguvu pamoja na tabia ni sahihi kutawala, na kwa vile anataka tuwe washirika wake katika kiti chake cha enzi kwa misingi ileile kuwa yeye alishinda na ameketi katika kiti cha enzi cha baba, hapo nasi inabidi tuwe washindi ili tuketi pamija naye. Na mateso haya madogo ya muda tunayojipatia sasa si kitu ukilinganisha na utukufuule mkuu ambao utafunuliwa kwetu wakati atakapokuja. **(2Korintho 4:17-18)** Oh ni hazina yz jinsi gani iliyowekwa kwa ajili ya wale ambao wako tayari kuingia katika ufalme wake kupitia dhiki nyingi. ***(matendo 14:22)*** [12]

Sasa ufunuo 3 ule mstari wa 21, tunasooma hivi " Yeye ashindaye niktampa kuketi pamija name katika kiti change cha enzi kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na baba yangu katika kiti chake cha enzi yeye aliye na sikio na ssikie neno hili ambalo roho ayaambia makanisa"

Je uliweza kuona ule mpangilio wa jambo hilo? Kuketi pamoja name siyo juu ya kiti change bali ndni ya kiti change" ndani ya kiti changu ni katika himaya yake na sasa kama vile ambavyo kristo ndiye mtawala, mtawala kwenye kiti cha enzi wakati huu wa sasa, katika himaya yote ya Mungu, kadhalika ndivyo kanisa litakavyokuwa pamoja naye, katika himaya yake, katika himaya yake yote. Unaona? Siyo juu ya kiti changu cha enzi lakini "Ni ndani ya kiti change cha enzi, unaona? Himaya yake inafika wapi? Kiti cha enzi kiko katika himaya. Na himaya inaenda mpaka ile mipaka ya yote inakoishia. Na hii ni kutoka milele mpaka milele, Hebu wazia hilo! [13]

Unaona Yule bibi arusi yuko pamoja naye katika kiti chake cha enzi, kwa kuwa yeye bibi arusi atahukumu ulimwengu-atakuwa ameketi katika hukumu pamoja naye. Hivyo ndivyo hasa Dnieli alivyoona.

Danieli 7:9-10" nikatazama hata viti vya eenzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, nanywele za kichwa chake cha enzi kilikuwa

na miali ya moto na gurudumu zake na moto uwakao.mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake, maelfuelfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake hukumu ikawekwa na vitabu vikafunuliwa "

Unaona ni mahali palepale, kwa kuwa maelfuelfu ambao walimtumikia yeye ni bibi arusi, kwa maoni ni nani anayemhudumia mume, ila mke wake? [14]

Mungu alituma siku ya pentekoste , Yule Roho mtakatifu kutawala ndani ya mioyo ya watu na kutawala katika maisha yake. Haikumaanishwa kamwe kwaa mtu kumtawala mtu mwingine. Lakini mtu anataka kutawala juu ya mtu, na mtu anataka mtu atawale juu yake, hamtaki Mungu awe mtawala wake. [15]

Sasa, tuanzapo kujifunza hili, kusudi langu sio kuja hapa kwa ushirika pamoja na ninyi watu, ambalo napenda kulifanya hilo lakini kama nikiwa na nafasi ya kufanya hilo. Nitakuja nyumbani kwako, na kukupa mkono , nakuzungumza na wewe na kukaa. Na kula chakula pamoja nawe, na kukaa chini ya mti wenye kivuli, na kuzungumza na kuwa naushirika kwa muda kidogo, lakini tunapokuja hapo, tuko hapa kwa kusudi maalumu. Hii ni nyumba ya masahihisho, hapa ni kwenye kiti cha enzi/ hukumu. Hapa ni kiti cha enzi cha Mungu, na hukumu inatendeka katika nyumba ya Mungu***. (Petro 4:17)*** nahapo ndipo tunapokusanyika pamoja katika upendo, wa mtu mmoja wa mwingine, kwa maana ni wakristo tuu wanaoweza kupenda, lakini hapa tunakuwa chini ya uongozi wa Roho mtakatfu, Roho mtakatifu yuko katikati yetu. Na tuko hapa kuweza kuchukua maonyo mioyoni mwetu. Kuona jinsi tulivyo wapungufu katika sehemu mbalimbali, mapungufu yetu. Na jinsi tuwezavyo kupanda na kuwa pale panapotupasa, tufike pale tupaswapo kuwa sasa. Tuko wapi na ni wapi tunapaswa kuwa nahilo ndilo tunalojifunza . wahuduma wanajifunza hizo sehemu, kwa ajili ya watu wao, kile kinachopunguka, hapo sasa wanaanzia hapo. Karibuni sasa, nafikiri kuwa kanisa pengine linapaswa kuchukua hatu a ya juu kidogo katika wakati huu. [13]

Sasa nataka kusema kuwa ninaamini katika uongozi (rum8:14). Lakini sio uongozi wa watu ambao ninaamini. Ninaamini juu ya uongozi wa Roho mtakatifu akija kupitia lile neno(kolosai 1:18-20) ninaamini pia , kwamba Mungu ameweka watu katika kanisa watu ambao wana vipawa walvyopewa na roho nao wataliweka kanisa katika utaratibu ***(waefeso 4:11-16)*** naamini hilo. Naamini pia kuwa lile kanisa linatawaliwa na watu ambao Mungu anawatuma kuliongoza. Lakini yale mamlaka ni kwa Neno, kwa hiyo sio watu hasa wanaotawala bali ni Roho wa Mungu, kwa maana lile neno na Roho ni moja. [16]

Mabata yatakusanyika pamoja kila mmoja wao nao watamkubuka kiongozi mmoja. Pale watajua kwa namna Fulani, sijui vile wanavyofanya. Lakini wao wanafahamukuwa huyu dume mdogo ni kiongozi nao wanakusanyika pamoja na kulia kumzungumka Yule bata mdogo na huruka juu hewani naye hajawahi kuondoka hapo hata, lakini ataenda hapo moja kwa moja mpaka Louisiana au Texas kadiri ya anavyoweza kwenda kule kwenye mashamba ya nyanya. Unaona? Kabla hawajaruka kuondoka katika makao yao ya nyumbani walipozaliwa mwaka ule , wanaungana pamoja. Amina! Unaona hilo? Wanalia na wanazungukia kiongozi wao. Tatizo la hilo ni kuhusu mtu, hawajui kiongozi wao atapiga kelele kuzunguka edhehebu, watapiga kelele kuzunguka askofu au mtu, lakini hawataki kuzmzunnguka kiongozi wao Yule Roho mtakatifu na lile neno. Unaona ? wanasema " oh Vema, ninaogopa nitakuwa kama aliyerukwa na akili kidogo,

naogopa nitapiga hatua kwa njiah iyo”  oh upo hapo.! Ni vipi kama Yule bata mdogo alisema “ sipendelei namna anavyoweka manyanya yake siamini kama nitamfuata yeye” yeye angekufa na kuganda kwa baridi. Utakutwa pale, kama huondoki nalile kundi pindi linapoondoka linalinganisha lenyewe pamoja. Na hilo ni tendo la kimaumbile linafanya hio.

Mabata yanajiunganisha yenyewe pamoja , wanapiga kelele kumzunguka Yule kiongozi wao wanafanya jambo hilohilo. [17]

Waebrania 13:17 “wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowambia eno La Mungu tena kwa kuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, igeni imani yao,. Baba wa mbinguni, Yule adui anaenda hukimbia adui ameshindwa. Yesu Kristo anaishi na kutawala. Shetani ameshindwa vita hivi! Yesu Kristo ameshinda ni mshindi. Wewe umewekwa wazi. Wewe ni mdanganyifu tu, na tunakuita uondoe mkono wako, kwa upendo wa msalabani. Toka kati ya hawa watu, katikajina La Yesu Kristo, na watoke hawa watu na uwaachie huru. [18]

**Nukuu za kingereza**

[1] Ufunuo wa Yesu Kristo CAB UK.35-30

[2] Umoja wa Mungu mmoja katika kanisa (58-1221E) Aya 45

[3] Lile Pengo (63-0317E) Aya 99

[4] Ufunuo wa sura ya 4 mstari wa 2 (61-0101) Aya 237

[5] Kama tai asambaratishavyo kiota chake (59-0815) Aya E-71

[6] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63-0728) Aya 233-240

[7] Kristo anatambuliwa kwa namna ileile katika vizazi vyote (64-0415) Aya 10-12

[8] Jehova jire sehemu ya 1 (64-0402) Aya 106

[9] jehova jire sehemu ya 3 (60-0803)Aya E 39

[10] Wkati wa kanisa la Thyatira (60-1208) Aya 36

[11] Maswali na majibu (62-0527), COD Aya 723

[12] Wakati wa kanisa wa Smirna cab uk. 117

[13] Nawezaje kushinda (63-0825) Aya 33-36

[14] Wakati wa kanisa la sardi CAB UK 275

[15] Mfalme aliyekataliwa (60-0515M), uk 9-10

[16] Wakati wa kanisa wa efeso CAB uk 93

[17] Kuunganisha wakati wa Ishara (63-0818) Aya 82-84

[18] Ishara ya wakati huu (63-1113) Aya 124.

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 16 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebeievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili,  andika kwa: Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe -  Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*